



REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

THIRD ASSEMBLY-THIRD SESSION

THE HANSARD

Tuesday, 25th June 2024

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 9:30 a.m.*

[The Temporary Speaker (Hon. Stephen) in the Chair]

PRAYER

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

VISITING STUDENTS FROM ARABUKO FOREST HIGH SCHOOL

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Hon. Members, I would like to acknowledge the presence in the public gallery this morning of students from Arabuko Forest High School.

The students are here for a study visit to appreciate the legislative procedures, practices, traditions and parliamentary proceedings. I request that each person stand when called upon so that they may be acknowledged in the parliamentary tradition and practices. I will start with the students first: -

1. Rajab Mohamed
2. Hussein Noor
3. Maslah Abdi
4. Abbas Mohamed
5. Said A. Shebwana
6. Swaleh Salim

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

7. Ahmed Bwana
8. Jaffar Sairiamu
9. Martah Rashid
10. Siraj Mohamed
11. Mohamed Moti
12. Murshid Muhumed
13. Naaman Gonzi
14. Answar Said
15. Hamza Aden
16. Abdile Mohamed
17. Mohamed Hussein
18. Sifa Chengo
19. Muktar Muhumed
20. Bashir Musa
21. Osman Garane
22. Ahmed Harun
23. Abbas Suleiman
24. Abdiaziz Mohamed
25. Mselem Yahya
26. Esam Abdihakim
27. Salim Said
28. Mdathir Sheikh
29. Dhulkifli Yusuf
30. Abdulrazak Fauz
31. Abdi Mustapha
32. Abdullahi Amin
33. Mohamed Abdalla
34. Muadham Fat-Hi
35. Ahmed Duale
36. Hussein Ali
37. Abdullah Abdi
38. Hamid Maulana
39. Abdisalam Hassan
40. Osman Buthul
41. Mohamed Mwero
42. Ahmed Nassir
43. Muadh Ali
44. Said Noor Hussein
45. Mohamed Mansour
46. Musab Swaleh
47. Siraj Mohamed
48. Abdulkadir Mahamud
49. Khalfan Omar

The following two teachers have accompanied the students:

1. Nyong'o Mark
2. Keraa Kelvin

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

On behalf of the County Assembly of Kilifi and on my own behalf, I welcome them to the County Assembly and wish them well. Thank you.

Waheshimiwa, ningependa kuchukua fursa hii kumkaribisha mheshimiwa ambaye shule ambayo imetutembelea iko kwa wadi yake na ni mheshimiwa Hassan. Karibu uwaeleze mawili matatu kwa wanafunzi wako. Mheshimiwa Elina Mapenzi ataongea badala ya mheshimiwa Hassan.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Asante, mheshimiwa Spika. Nimesimama kwa niaba ya mheshimiwa Hassan ambaye anawakilisha Wadi ya Matsangoni ambapo wanafunzi wale ndiko wanakotoka. Mimi nikiwa mzaliwa wa maeneo hayo pale Roka Maweni, nimeteuliwa katika Bunge hili na jina langu naitwa Elina Mapenzi Samini.

Nataka kuchukua fursa hii kwa niaba yake kuwakaribisha katika Bunge letu la Kaunti ya Kilifi na pia kuwaambia mkaribie na kuwaeleza machache jinsi tunavyofanya hapa Bungeni. Wakati tukiwa kule nje tunatafuta kura huwa tunatumia lugha ya kisiasa hiyo ni sajili moja wapo katika somo la Isimu Jamii mnalofunzwa kule shuleni.

Mnapoangalia sajili, kuna sajili za aina mbili. Kuna muktadha rasmi na muktadha usiokuwa rasmi. Ndani ya ule muktadha usio kuwa rasmi kuna sajili ya siasa. Katika ule muktadha rasmi kuna sajili ya Bunge. Kwa hivyo, sisi tukiwa uwanjani tukitafuta kura huwa tunatumia ile sajili ya siasa ambayo sio muktadha rasmi.

Tunavyoelewa kwamba muktadha sajili ni matumizi ya lugha kulingana na muktadha. Kwa hivyo, tukiketi hapa sasa tunaongozwa na sajili rasmi ambayo ni sajili ya Bunge. Matumizi ya lugha hapa yanakuwa rasmi. Hatuborongi sarufi, hatutumii *propaganda*, kila linalozungumziwa hapa ni la uhakika na kwa mujibu wa sheria kwa sababu tunaongozwa na sheria tukiwa hapa Bungeni tofauti na tukiwa kule uwanjani.

Sitaki niwachoshe nichukue muda mwingi. Tuna mambo mengi ya kufanya katika Bunge hili. Karibuni sana na mnaporudi kule shule muwe na nidhamu. Mtilie maanani masomo, mfuzu na hiyo ndio furaha ya mzazi anayelipa ile karo yako. Asanteni.

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Asante sana, mheshimiwa Elina Mapenzi. Ni matumaini yangu ya kwamba wanafunzi mtashika yale ambayo mheshimiwa amejaribu kuwaelezea. Niko na mheshimiwa Ibrahim Abdi Athman, tafadhali ongea.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Asante, Bw. Spika, kwa kunipatia nafasi hii. Nataka kukaribisha wanafunzi wa Arabuko Sokoke lakini kabla sijawakaribisha, Bw. Spika, umetangulia kusema umenipa nafasi mimi kama Ibrahim Abdi Athman, nakuomba Bw. Spika uniite mheshimiwa na pia unipe jina langu ndio wanafunzi wasome.

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Asante, mheshimiwa Ibrahim Abdi Athman, akiwa ni Kiongozi wa Wengi, Bunge la Kaunti ya Kilifi. Tunakuenzi sana na unatufanyia kazi nzuri. Karibu sana na nimetoa hiyo, endelea tafadhali.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Asante. Nilikuwa nataka kuwaonyesha wanafunzi ya kwamba tunarekebisha pia sisi hapa ndani ya Bunge kama vile wanarekebisha kule shule. Ninashukuru kupata nafasi hii kuongea na kuwakaribisha wanafunzi kwanza. Kama mlivyoambiwa, mimi kwa jina naitwa Ibrahim Abdi Athman. Ni Mwakilishi wa Wadi ya Watamu Eneo Bunge la Kilifi Kaskazini ambayo shule hii ya Arabuko Sokoke iko. Mimi ni Kiongozi wa wengi Bungeni. Kule kwenu mko na viranja wa darasani sasa mimi ndio Kiranja wa Bunge.

Nataka kuwashukuru nyinyi wanafunzi na shule kwa jumla. Hii ndio shule ambayo sisi kama waheshimiwa ikiwa tunaenda kwa mikutano ya siasa ama ya kuelembisha wanafunzi,

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

tunaiga mfano na tunawaelezea mfano wa Arabuko Sokoke. Arabuko Sokoke ndio shule pekee katika Jimbo letu la Kilifi imeinua jina la Kilifi kielimu. Hiyo mimi nataka kuwapongeza sana wanafunzi. Vile vile, nidhamu ya Shule ya Arabuko Sokoke iko hali ya juu sana. Msione sisi kama viongozi hatufwatilii; tunawafwatilia sana na tunawashukuru sana kwa nidhamu mnayoweka katika shule. Mmefanya jina la Kilifi kutambulika katika ngazi ya Taifa letu la Kenya kieleimu. Kwa hivyo, ninawapongeza sana vijana wangu. Kitu muhimu ni kuzidi kuwa na nidhamu, mushirikiane ndio mtapata ushindi katika maisha yenu. Vile mliyoy, muendelee kuwa hivyo hivyo.

Ndani ya Bunge hili, kama nilivyotangulia kusema mimi ndio Kiongozi wa Wengi na Bungeni tuko waheshimiwa 51. 35 walichaguliwa na wananchi, kumi na nane walioteuliwa kwa vyama (*nominated*) yaani Wabunge maalum. Hapa tuko na vyama tofauti tofauti. Tuko na ODM (*Orange Democratic Movement*) ambao ndio wengi, tuko na UDA (*United Democratic Alliance*), PAA (*Pamoja African Alliance*) na pia tuko na *Independent* wale waheshimiwa waliochaguliwa bila vyama wako hapa. Kitu muhimu nataka kusema ni kwamba huko shuleni kwenu lengo lenu nyinyi ni kuboresha elimu.

Sisi hapa lengo letu ni kuboresha elimu na maisha ya wananchi. Kwa hivyo, kitu ni ushirikiano. Sisi huwa tunasikia uchungu kama viongozi tukisikia wanafunzi wamechoma shule. Ni jambo linatukera sana. Mwanafunzi ukiwa na changamoto kamuone mwalimu wako na mambo kama hayo yatatatuliwa. Kwa hayo machache, ninawakaribisha na Mungu awape akili bora za kuinua jina la Kilifi.

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Asante mheshimiwa kwa mawaidha mazuri kwa wanafunzi. Mheshimiwa Kea.

Hon. Kea: Thank you for giving me this opportunity. I stand on behalf of the English-speaking people and Members of this County Assembly to inform you that we use both Swahili and English. As the Leader of Majority has put it, you have head-boys; I want to correct him, that nowadays they use 'Presidents' and 'Governors'. As you said we should correct one another; you can have your dose on that.

I want to thank the students and teachers of Arabuko Sokoke for considering the Kilifi County Assembly as your area of education. I am a neighbouring MCA (Member of County Assembly) of Kibarani Ward and there are Tezo and Matsangoni. I am so close to you. I normally see your school whenever I pass every morning or afternoon coming to the Assembly and I am happy to inform you that you are one of the most disciplined schools in our Kilifi North Sub-County and I want to keep on encouraging you to keep on doing that and put more effort on your education and that you may be better people than we are today.

All the names that have been mentioned I have gotten one; Aden Duale. I think he is one of the public figures and I want to believe that you are going to be more vocal and powerful than the current Minister with that name.

I want to congratulate you hon. Elina Mapenzi for your good Swahili. I did not know that you are a Swahili teacher, but I want to believe the students have gotten something from you on the words of *muktadha* and so many others. Thank you, very much and welcome to Malindi and the County Assembly of Kilifi.

Hon. Juma: Asante kwa hii nafasi. Jina langu naitwa Juma Chengo. Mimi ni miongoni mwa wale wachache ambao Kiongozi wa Wengi Bungeni alisema kwamba wamekuja bila kuzingatia chama. Tuko wanne hapa Bungeni na mimi nawakilisha Mnarani. Jambo ninalotaka kuwajulisha ni kwamba hapa mtu yoyote anaweza kuingia. Tengezeni vizuri CV (*Curriculum Vitae*) zenu na mtaweza kujikuta hapa na maeneo mengine. Asante sana, Bw. Spika.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Nachukua fursa hii kuwashukuru walimu na wanafunzi pamoja na waheshimiwa ambao wamechangia kuwapa mawaidha wanafunzi wetu. Naomba wanafunzi wazingatie haya waliyofunzwa hapa na waheshimiwa.

PAPERS LAID

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Thank you, Mr. Speaker, Sir. Today, being Tuesday, 25th June 2024, I beg to lay the following Papers on the Table: -

- 1) Fiscal and Land use plan for Vuma Trading Centre PDP No. 883.KLF.1.2019
- 2) The Kilifi County Youth Development Policy 2022-2026 from the Department of Gender, Culture, Social Services, Sports and Disaster Management.

(Hon. Ibrahim laid the documents on the Table)

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Asante, mheshimiwa Ibrahim. Ripoti ya kwanza itaenda kwa Kamati ya *Lands, Physical Planning* na ya pili itaenda kwa *Youth, Gender and Culture*.

STATEMENT

STATUS OF KWA KIJALA AND KAWALA BOREHOLES

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): *Statement* ambayo iko hapa ililetwa na mheshimiwa Naphtali Nyae Kombo na kwa sababu leo hatuko naye hapa, naomba irudishwe kwa Kamati ya *House Business Committee* ili ipangiwe muda tena na muhakikishe kuwa mukiileta tena mwenyewe atakuwa Bungeni.

(Statement deferred)

ADJOURNMENT

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Kwa kuwa hakuna la ziada, kikao hiki kimefungwa hadi saa nane na nusu. Asanteni sana.

The House rose at 9:51 a.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*